Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 3, Issue 4

14th Dhul-Qa'dah 1431

22nd October, 2010

Naseeha Kwa Wenye Nia Ya Kwenda Hajj

Mtayarishi: Sheikh Muhammad Naasir-ud-Deen al-Albaani (رحمه الله)

Zifuatazo ni baadhi za vipande vya naseeha na vidokezo vya faida nilivyowapa Waislamu ambao waliokurubia kutekeleza Hajj (kwenda kuhijji Makka)

KUDUMISHA TAQWAA

Mwenye kuhijji ni lazima awe na taqwaa (uchaji na unyenyekevu) mbele ya Mola wake. Ni lazima ajitahidi kujiepusha na Aliyoyakataza. Amesema Allaah: **"(Wakti wa) Hijja ni miezi yenye kujulikana (Shawwal, Dhul-Qa'da na siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhul-Hajj). Na yoyote inapomlazimu yeye Hijja basi asitamke maneno machafu wala kufanya ma'asia na kubishana katika Hijja."** [al-Baqarah 2:197]

Na Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Mwenye kuhijji na akajiepusha na mazungumzo machafu na akajiepusha na vitendo viovu atarudi akiwa safi kutokana na madhambi kama alivyokuwa siku alipozaliwa na mamake."*

Iwapo atafanya hivyo, basi Hajj yake itakuwa imefuzu (mabroor). Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hajj ambayo ni mabroor haitokuwa na malipo isipokuwa Pepo"*.

Kwahiyo, ni waajib kuwatahadharisha watu dhidi ya baadhi ya ukiukaji ambao hufanywa na wengi, emma kwa ujinga au kwa makosa.

KUJIEPUSHA NA SHIRK

Tumewahi kuwaona watu wengi (katika wakati wa Hajj) wakiathiriwa na janga la Shirk (kuwahusisha washirika na Allaah (سبحانه وتعالى)). Kwa mfano, wanamswalia asiyekuwa Allaah (سبحانه وتعالى) kwa ajili ya kuwaondoshea dhiki, wanataka msaada kutoka kwa Mitume waliokufa na watu wema, wanawaomba wao badala ya kumuomba Allaah (سبحانه وتعالى), na wanakula viapo kwa kuwapitia wao kwa ajili ya kuwatukuza. Kwa kufanya vitendo aina hiyo huwa wamezibatilisha kabisa hajj zao, kama alivyosema Allaah: **"Wallaahi ukimshirikisha Allaah wallaahi zitapomoka, zitapomoka amali zako."** [az-Zumar 39:65].

KUJIEPUSHA KUZINYOA NDEVU

Baadhi ya wanaume hujirembesha nafsi zao kwa kujinyoa ndevu. Hili ni tendo ovu lililokusanya ukiukaji sampuli Nne tafauti za Uislamu.

a.Ni kui'asi amri ya wazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba tuwachane na ndevu.

b. Ni kuwaiga makafiri.

c. Ni kubadilisha Uumbaji wa Allaah.

d. Ni kujifananisha na wanawake.

WANAUME NI LAZIMA WAJIEPUSHE NA KUVAA DHAHABU

Kuvaa pete za dhahabu kumeharamishwa kwa wanaume. Ile sampuli ya pete ambayo leo inaitwa pete ya uposi.

KUKUSUDIA SAMPULI YA SAWA YA HAJJ

Ni nadra sana siku hizi kwa wenye kuhijji kuleta *hadee* (mnyama wa swadaka) pamoja nao, kama alivyofanya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hapana lawama kwa jambo hilo. Hatahivyo, yoyote ambaye hakuja na *hadee* na akusudie kutekeleza *Hajj ya tamattu'* - na isiwe ni *Hajj ya qiraan* wala ya *ifraad*. Asipofanya hivyo, atakuwa anakwenda kinyume na kitendo na amri alizokuja nazo Mtume (صلى الله عليه وسلم). Baadhi ya sababu zake ni:

a) Hivi ndivyo ambavyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyowaamrisha Maswahaba zake wafanye alipofikiya mwishoni (mwa maisha yake).

b) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikasirika sana pindi baadhi ya Maswahaba zake walipowacha kutekeleza amri yake palepale kubadilisha niya zao kutoka kwenye Hajj kwa '*Umrah*.

c) Baadhi ya Maswahaba walipouliza iwapo alilifanya hilo kwa mwaka huo peke yake au ni la milele, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivishikanisha vidole vyake pamoja na akasema: *"'Umrah imeingiana ndani ya Hajj mpaka siku ya*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

Naseeha Kwa Wenye Nia... 1– 3

Damu Asilia za wanawake 4

Naseeha Kwa Wenye Nia Ya Kwenda Hajj

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kufufuliwa—bali, milele na milele, bali milele na milele."

d) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuamrisha bintiye Faatimah na wakeze (رضي الله عنهم) wajihalalishe (waondoke kwenye hali ya *ihraam)* baada ya kukamilisha '*Umrah* ya Hajj.

e) Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) alikuwa akisema: "Yoyote mwenye kufanya *twawaaf* (kutufu) kuizunguka Nyumba basi atakuwa amejiondoa kwenye *Ihraam*. Hii ndiyo Sunnah ya Mtume wenu, hata kama inawakirihisha. Msingi wa haya ni maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kwa hakika Allaah ameziunganisha 'Umrah na hii Hajj yenu; kwahivyo yoyote atakaewasili, na kutekeleza twawaaf ya Nyumba, na akenda baina ya Swafaa na Marwah, atakuwa amejihalalisha (atajiondoa kwenye Ihraam) - isipokuwa kwa yule aliyekuja na hadee wake."* Kwahiyo, kila ambaye hakuja na mnyama na alete talbiyah (alinganie mwito) yakwamba yeye anakwenda kutekeleza 'Umrah wakati wa miezi mitatu ya hajj.

Na kwa yule ambaye aliyeitangaza niya yake ya kutekeleza *Ifraad* au *Qiraan*, kisha baadae akasikiya kuhusu amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) basi na aibadilishe niya yake na kuwa '*Umrah*, na *aitwi'i* amri hiyo kwa haraka—hata ikiwa ni baada ya kuwasili Makkah na kutekeleza *sa'y* baina ya *Swafaa* na *Marwah*. Na ajiondoe kwenye hali ya *Ihraam* na baadae atie niya ya hajj ifikapo siku ya *Tarwiyah* (tarehe 8th ya Dhul-Hijjah). Ameamrisha Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi Mlioamini! Itikieni mwito wa Allaah na wa Mtume anapowaita muamini."** [al-Anfaal 8:24].

Amri hii haipingani na yaliyopokewa kutoka kwa 'Umar (رضي الله عنه) na wengineo kuwa Ifraad ni bora, kwa sababu inatibidi tuzingatie yakwamba walikuwa wakileta wanyama pamoja nao. Na pia nimeona vilevile yakwamba Ibn Taymiyyah ameieleza nukta ya 'Umar kumaanisha kuifanya safari ya 'Umra kando na safari tafauti ya hajj.

KULALA MINAA NA MUZDALIFAH

Mtu na asipuuze kukaa Minaa katika usiku unaotangulia Siku ya 'Arafah. Hili ni jambo la waajib lililofanywa na kuamrishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye amri yake: *"Chukuweni kutoka kwangu ibada yenu ya hajj."*

Pia, mtu anatakiwa akae Muzdalifah katika usiku utakaofuata mpaka amalize kuswali swala ya fajr hapo. Mtu akikosa kukaa hapo (kutokana na kuchelewa njiani) basi angalau itamlazimu aswali fajr hapo, kwa vile hilo ni waajib zaidi—bali, hiyo ni *rukn* (nguzo) ya hajj kulingana na rai iliyosawa ya wanavyuoni. Hatahivyo, jambo hilo haliwahusu wanawake na wanyonge, kwani wao wameruhusiwa kuondoka kutoka Muzdalifah baada ya katikati ya usiku, kama itakavyojadiliwa baadae.

KUJIEPUSHA KUPITA MBELE YA WANAOSWALI

Ni lazima mtu ajiepushe kwa tahadhari kupita pasi na kizuizi mbele ya mwenye kuswali. Hili linawahusu wale wenye kuswali katika *al-Masjid ul-Haraam* (msikiti mtukufu wa Makkah) na vilevile katika misikiti mengine na sehemu nyengine; amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Lau angelijua mwenye kupita mbele ya mwenye kuswali hatia itakayomsibu (ya madhambi), basi angeliradhiwa kungojea (kwa kusimama) kwa arubaini kuliko kupita mbele yake."* Mmoja wa wapokezi wa hadeeth hii alikuwa na shaka iwapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitaja masiku, miezi, au miaka baada ya kutamka arubaini. Hili ni andiko la ujumla linalowahusu kila mwenye kuswali au kupita mbele ya mwenye kuswali. Hakuna hadeeth iliyo swaheeh yenye kuiepusha *al-Masjid ul-Haraam* kutoka kwenye hukmu hii. Kwahiyo, kama kuswali mahali pengine popote, mtu ni lazima aswali hapo kuelekea sutrah. Hii imetokana na ujumla wa kawaida wa asili ya hadeeth inayohusiana na sutrah, na vilevile riwaya makhsusi zilizo swaheeh kuhusu vitendo vya Mswahaba (رضي الله عنهم). Kwa mfano, imeswihi kupokewa yakwamba, wote wawili, Anas na Ibn 'Umar walikuwa wakiweka Sutrah walipokuwa wakiswali katika *al-Masjid ul-Haraam* (Angali kwenye *Hajjat un-Nabee* cha al -Albaani).

UWAJIBIKAJI WA WENYE KUJUA

Wakati wa hajj unapowadia, wanavyuoni na wenye fadhla na wawafunze waliokuja kuhijji, kila wanapo onana nao, nguzo na hukmu za hajj kulingana na Kitaab na *Sunnah*. Zaidi ya hayo, hilo lisiwazuie kulingania kwenye Tawheed, ambayo ndicho kiini cha Uislamu; hiyo ndiyo sababu ambayo kwayo wametumilizwa Mitume na Vitabu kuteremshwa. Watu wengi ambao tuliowaona, na hata wale ambao waliotarajiwa kuwa na 'ilmu, wako katika ujinga mtupu wa maana halisi ya *Tawheed* na Sifa za Allaah. Vilevile wao hawana wajualo kabisa kuhusu yenye kuleta michafuko ya mifarakano baina ya Waislamu, ambayo yaliyosababishwa na kutafautiana kwa madh-hab zao (mtazamo katika kufikia hukmu za ki-Islamu) na vyama. Kwahiyo, wao wanapuuza kujishughulisha na kuwaunganisha pamoja na kuziunganisha swafu zao juu ya Kitaab na Sunnah katika nyanja zote: katika Imani ('aqeedah), hukmu (ahkaam), mapatano ya kibiashara, tabia, siyasa, hali ya kiuchumi na mas'ala yote mengine ya kimaisha.

Ni lazima wakumbuke yakwamba sauti zozote zenye kupaazwa, au hatua yoyote inayofanywa kwa malengo ya kuleta mabadiliko, yatakayoegemezwa juu ya kitu

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

Naseeha Kwa Wenye Nia Ya Kwenda Hajj

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

chochote kisichokuwa msingi huu imara na njia iliyonyooka, utazidi kuleta mgawanyiko zaidi na kudhoofika kwa Waislamu, na utazidisha kuaibishwa kwao na kudhalilishwa. Hali waliyonayo hivi sasa ni dalili iliyo dhahiri ya nukta hii, na Allaah ndiye Mwenye kuombwa msaada.

Wakati wa hajj, inaruhusiwa kujadiliana kwa njia nzuri—kama inavyohitajika. Lililokatazwa ni kufanya mijadala isiyo na manufaa kuthubitisha jambo lenye makosa, hili haliruhusiwi hata nje ya hajj—kama ambavyo kufanya madhambi katika wakati wa hajj na usiokuwa huo. Sampuli hiyo ya mijadala isiyo na manufaa haistahili kutokana na amri ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Waite (watu wote) katika dini ya Mola wako kwa usemi wa busara na mawaidha mazuri. Na bishana nao (wanaokukhalifu) kwa yaliyo bora."** [an-Nahl 16:125].

Hatahivyo, iwapo itadhihiri kwa *daa'iyah* (mlinganizi, mwenye kufanya *Da'wah*) yakwamba hapana faida ya kujadiliana na mtu fulani, kwa sababu ya kujinatisha kwa mtu huyo kiupofu juu ya madh-hab yake au rai yake binafsi, na kwamba kuendelea kujadiliana nae kutaleta matokeo yasiyoruhusiwa, basi ni bora kukoma kujadiliana, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mimi ni mdai wa nyumba iliyo pambizoni mwa Pepo kwa yule mwenye kuwacha mijadala hata kama yuko kwenye usawa."*

HAPANA UZITO HAPANA UZITO!

Daa'iyah na ajitahidi kufanya mambo kuwa mepesi kwa watu kwa ujumla na kwa mahujjaji hususan. Wepesi huo, kama ujulikanavyo, ni miongoni mwa misingi asili ya sharee'ah, maadamu hakuna maandiko yaliyo dhidi ya wepesi kama huo. Hatahivyo, iwapo kuna andiko makhsusi, basi uzembeaji kwa kutegemea rai tupu hairuhusiwi tena. Huu ndio msimamo wa uadilifu wa kati na kati ambao unampasa kila *daa'iyah*, bila ya kujali uhakiki au pingamizi za watu, wakisema, "huyu ana mikazo mengi", au, "huyu ana huruma sana."

Kuna idadi ya vitendo vyenye kuruhusiwa wakati wa hajj, lakini baadhi ya mahujjaj wamezoea kujiepusha navyo kutokana na *fatwaa* zilizotolewa na baadhi ya wanavyuoni zenye kupingana na misingi iliyotangulia kutajwa, ambayo miongoni mwake ni:

1.Kuoga, pasi na haja kwa sababu ya ndoto ya kimapenzi (ihtilaam), hata kama ikihusisha kujipangusa kichwa—kama ilivyoswihi kupokewa kutoka kwa Abu Ayyub (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amfanya.

2.Kujikuna kichwa, hata kama hilo litasababisha baadhi ya nywele kung'oka. Hii imeashiriwa kwenye hadeeth iliyotangulia ya Abu Ayyub, na ni rai ya *Sheikh ul-Islaam* Ibn Taymiyyah (رحمه الله).

3. *Ihtijaam* [Hii ni aina ya utabibu wa ki-zamani unaohusu kuumika sehemu makhsusi za mwili au kichwa na kutoa damu], hata kama itahusiana na kunyoa kabisa baadhi ya nywele. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahi kufanyiwa katikati ya kichwa chake, hali akiwa kwenye Ihraam—na hilo haliwezekani bila ya kunyoa baadhi ya nywele. Hii pia ndiyo rai ya Ibn Taymiyyah—na vilevile ya wanavyuoni wa Hanbalee ambao, hatahivyo, itahitaji kuchinja (*fidyah*) kwa mwenye kufanya hivyo. Hawana dalili ya hayo, bali madai hayo yamekatiliwa kwa sababu ya kitendo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم). Lau kama angelitoa *fidyah*, mpokezi angelisema hayo; kwa kukosa kufanya hivyo ni ishara yakwamba hayakutokea hayo.; kwahivyo msimamo wa sawa ni ule wa Ibn Taymiyyah (رحمه الله).

4.Kunusa mimea yenye kunukia vizuri na kukata kucha—kama ilivyoshurutishwa na Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) na Sa'eed bin al-Musayyib.

5.Kujikinga kwenye kivuli chini ya hema au nguo iliyobebwa—kwa vile hii imeswihi kupokewa kutokana na kitendo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم). Ama kuhusu aliyoyapokea al-Baihaqee yakwamba 'Umar (رضي الله عنه) alimuamrisha mtu aliyefanya hivyo achinje, hiyo ni rai yake ambayo haiwezi kutumika kama dalili dhidi ya hadeeth hii iliyo swaheeh. Lenye kulingana na hili ni kujikinga na kivuli ndani ya Behewa la Ngamia [juu ya mgongo wake] katika siku za kale, au chini ya muavuli, au ndani ya magari katika mambo ya kisasa. Kuwajibika kutolewa *fidya* katika suala hili ni kuweka mikazo isiyokuwa na dalili. Hakuna tafauti baina ya kivuli cha hema (ambacho kilichotajwa kwenye Sunnah) na kivuli kutoka kwenye behewa la Ngamia na mfano wake, na hii imepokewa kama rai kutoka kwa Imaam Ahmad (رحمه الله). Baadhi ya watu hung'oa mapaa ya magari yao (ili wasiwe chini ya kivuli)! Huku ni kupinduka mipaka kwenye Dini bila ya ruhusa kutoka kwa Mola wa Walimwengu.

6. Kuvaa ukanda kuizunguka *Izaar* na kujifunga ikibidi, pia kuvaa pete, saa, miwani, au kujizingirisha shingoni vipochi vya pesa, hapana makatazo yoyote kuhusu hayo; licha ya hayo, baadhi ya riwaya kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) na 'Ataa' (رضي الله عنه) zinaashiriya kuruhusiwa kutumia vitu aina hiyo. Mambo yote haya yanakuwa chini ya misingi iliyotangulia. La ziyada, baadhi yake zimeungwa mkono na ahaadeeth zilizo swaheeh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kwa riwaya zilizopokewa kutoka kwa Maswahaba—na Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Allaah yuwawatakia wepesi. Na wala hawatakii uzito."** [al-Baqarah 2:185].

Kila Sifa njema ni zenye kumthubutukia Allaah, Mola wa walimwengu wote.

Maneno yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema, "ikiwa heidh ya kikweli ikianza", inaashiriya yakwamba hukmu ya mwanamke Mustahaadhah zitakuwa ni waajib juu ya mwanamke ambae, ikiwezekana, huwenda akawa na heidh (iliyo na mwanzo na mwisho).Hatahivyo, mwanamke asiyeweza kuingia mwezini, basi damu yake ni damu itokayo kwenye mshipa.

HUKMU ZA MUSTAHAADHAH

Kutokana na hayo ya juu yaliyowahi kutokea, sisi tushatangulia kujua ni lini damu itakapokuwa ni ya heidh na ni lini itakapokuwa ni ya istihaadhah.

Kwahiyo, pindi itakapothubutu kuwa ni damu ya heidh, itachukuwa hukmu za heidh, na pindi itakapothubutu kuwa ni damu ya istihaadhah, itachukuwa hukmu za istihaadhah kama inavyowajibika.

Nukta muhimu kuhusiana na hukmu za heidh tayari zishatajwa. Hatahivyo, kuhusu hukmu za istihaadhah, ni kama hukmu za kujitwahirisha. Hapana tafauti baina ya mwanamke atokwae na damu (Mustahaadhah) na mwanamke aliye twahara, isipokuwa kwa yafuatayo:

Kwanza: Ni waajib juu ya mwanamke mwenye kutokwa na damu kutawadha na kuswali kila inapofika wakati wa kuswali katika swala tano za faradhi, kila siku, hata kama hakukidhi haja ndogo (ya kukojoa) au hata (haja kubwa ya choo). Hii ni dalili kutoka katika hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomwambia Faatimah Bint Abu Hubaish (رضي الله عنهما): *"Kisha tawadha kwa kila swala ya faradhi."*

Kwa maana yakwamba (mwanamke huyo) na asitawadhe kwa ajili ya kuswali isipokuwa ufikapo wakati wa swala uliowekwa na wala asifanye hivyo kabla ya kuingia wakati.

Pili: Atakapokutawadha, kwanza na aoshe alama za damu kisha na ajifunge kwa kipande cha kitambara (kilicho wekewa chiniyake, pamba) kuzunguka pande zote za utupu wake ili iweze kuikinga damu. Hii na ifuatwe katika kuitikia mwito wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa Hamnah Bint Jahsh (رضي الله عنهما): *"Ningependekeza (ujifunge na) Al-Kursuf (pamba) kwa sababu huondoa (hufyonza) damu."* Akasema (Hamnah): "Kwa hakika ni nyingi zaidi ya hivyo." Akamjibu (صلى الله عليه وسلم): *"Chukuwa kipande cha kitambara."* Akaongezea: "Inatoka kwa wingi zaidi ya hivyo pia." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Basi Talaj'jamee"* (Yaani; ajifunge kibobwe kuzunguka kiuno chake kitakachozuiya lile pamba madhubuti kwenye tupu yake). Hakuna chochote chenye kumtoka kitakachomdhuru kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia Faatimah Bint Abu Hubaish (رضي الله عنهما): *"Jiepushe na kuswali wakati wa heidh, kisha jitwahirishe na utawadhe kwa kila kipindi cha swala, kisha uswali hata kama damu itakuturuzika na itone juu ya mkeka."*

Tatu: Kuingiliana Kimapenzi: Wanavyuoni wa ki-Islamu wamekhitilafiana kuhusu kuruhusiwa kwake. Rai iliyo sawa ni kwamba inaruhusiwa kwa sababu wanawake wengi (kumi au zaidi) walipata damu ya Istihaadhah wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake hawakuwakataza mume na mke kutekeleza tendo la kuingiliana kimapenzi. Kwa hakika, maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Jiepusheni na wanawake wakati wakiwa kwenye heidh."**

Ni dalili yakwamba ni wajib kujiepusha na kitendo cha kuingiliana kimapenzi peke yake na wanawake wakiwa kwenye ada zao za mwezi tu. Na kwa vile wanaruhusiwa kuswali halitakuwa wakiwa kwenye Istihaadhah, basi haitakikani kuwe na uzito wowote kujamiiyana kimapenzi. Kukataza tendo la kujamiiyana kwa kutegemea Qiyaas na hali ya heidh ni makosa, kwa sababu hali hizo mbili si sawasawa. Kwahiyo, Makisio hubatilishwa kupatikanapo tafauti za aina hiyo.

NIFAAS NA HUKMU ZAKE

Nifaas: Ni damu inayomtoka mwanamke mja mzito kutokana na mazazi. Huwenda itatokea wakati wa mazazi, baada ya mazazi, au kabla ya mazazi (kwa siku mbili au tatu ikiungana na kubana kwa misuli). Amesema Sheikh ul Islaam Ibn Taymiyyah: "Damu inayo onekana wakati mwanamke akianza kubanika misuli yake ni Nifaas na haitokoma kwa siku mbili au tatu. Kubanwa huku kwa misuli hufuatwa na mazazi au kinyume chake damu hiyo iliyotoka si Nifaas."

Wanavyuoni wamekhitilafiana iwapo kuna kikomo juu ya muda wake. Amesema Sheikh ul Islaam Ibn Taymiyyah: "Nifaas haina kikomo juu muda wake mrefu au mfupi. Tuchukulie kwa mfano mwanamke ameona mturuziko wa damu kwa zaidi ya siku arubaini, sitini au sabiini kisha mara damu hiyo ikasimama. Aina hii ya kutokwa na damu inaitwa Nifaas. Tuseme, hata hivyo, yakwamba damu hiyo imeendelea kutoka, kisha kiwango cha masiku arubaini kikawekwa kuwa ni damu ya Nifaas kwa sababu muda huu ndiwo muda unaokabiliwa kwa kawaida na wanawake wengi".

[Endelea Katika Makala Yajayo]

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفريقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net